# Kinachotutofautisha na wengine

Kinachotutofautisha na wengine ni kwamba mmiliki na mwanzilishi wa kampuni alisomea na kufanya kazi Marekani kwa miaka 12 katika makampuni makubwa ya kimataifa ya mabango na uchapaji jijini New York. Maarifa na uzoefu katika mazingira kama hayo sasa unaletwa kwenu nyote.

Tuna upendeleo kulinganisha na wengine kutokana na ufahamu wetu mkubwa wa kimataifa uliopatikana kwa kusafiri sana ili kuhudhuria warsha, makongamano na semina za kimataifa kuhusiana na ujuzi mpya wa mabango ya biashara na teknolojia ya LED.

Jambo la kuzingantia ni kwamba sisi ndio waasisi linapokuja suala la kuanzisha dhana za kisasa katika mabango ya biashara na utengenezaji wake kwa kutumia teknolojia ya kompyuta.

Tulianzisha dhana nyingi za kisasa za mabango ya biashara nchini wakati wengine wakiwa bado wanafanya kazi kama wachora mabango na wahunzi katika utendaji kazi wao.

Sisi ni Kampuni ya mabango ya biashara iliyopewa hati na Shirika la Viwango la Tanzania (TBS) kutokana na mabango yetu kukidhi ubora unaotakiwa wa viwango Kitaifa.

Sisi ndio kampuni pekee ya mabango ya biashara nchini kupewa hati ya mkandarasi DARAJA LA 1 iliyotolewa na CRB, shirika la kitaifa la usimamizi na udhibiti wa makandarasi.

Tunajivunia kuchukua tuzo mashuhuri Tanzania ya Makampuni 100 makubwa kwa miaka minane mfululizo na tumeainishwa kuwa katika makampuni 10 makubwa nchini.

Tuna wabunifu wenye ujuzi na uzoefu wa hali ya juu, mafundi na watenda kazi wengine kutoka nje na hapa nyumbani, wenye uzoefu wa kimataifa katika nyanja mbali mbali za utengenezaji mabango kwa njia ya kidijitali, CNC, maroboti na wenye ujuzi wa uzalishaji kwa mitambo ya kujiendesha yenyewe. Pia tunatoa mafunzo ya mahala pa kazi ili kuwanoa wafanyakazi kwa kufanya kazi nzuri na ya kiwango cha ubora wa hali ya juu katika ngazi zote za uzalishaji.

Tunayo Idara ya Ubunifu na Utafiti na Maendeleo (R&D) yenye vigezo vya juu sana vya majaribio na mfumo wa udhibiti.

Ni mwanachama wa ISA (*International Sign Association* ) ya Marekani na mara kwa mara tunahudhuria mikutano yao ili kwenda na wakati katika medani ya mabango ya biashara na huduma nyingine shirikishi.

Tuna eneo la kiwanda la ukubwa wa futi za mraba 25,000 (2,300 sq m) na maduka mawili ya kuonesha bidhaa zetu , moja likiwa katika mtaa mmoja mashuhuri katikati ya jiji.

Sisi ni mwajiri atoaye fursa sawa kwa wote na tuna sera dhidi ya ubaguzi. Pia tunayo sera dhidi ya rushwa, sera ya usalama mahala pa kazi na sera nyingine zinazohusiana na kazi. Tuna bima ya Shilingi milioni 100 dhidi ya kutenda makosa ya kikazi.

Tuna sera mbali mbali za usalama, mazingira, maadili na mambo muhimu ambazo zinatuongoza katika nyanja zote za kazi yetu, uzalishaji, usimikaji, Mahusiano na Jamii, Rasilimali Watu, manunuzi na mauzo.

Sign Industries Ltd.
PROFESSIONAL SIGNAGE & BRANDING